

**HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA
SHULE YA MSINGI MATONDO
MTIHANI WA MAJARIBIO DARASA LA NNE MWEZI JULAI -2024
MAARIFA YA JAMII**

JINA LA MWANAFUNZI _____ MUDA: 1:00

1. Kujibu kipengele (i) - (viii) chagua jibu sahihi na kuandika herufi ya jibu katika kisanduku kilichowekwa.

- i. Gimba linaloumbwa na miamba ambalo hulizunguka jua kupitia njia maalum huitwa?
A. Mwezi B. Jua C. Sayari D. vimondo
- ii. _____ umezungukwa na sayari nane na vitu vingine kama Asteroidi, Kometi na meteroidi.
A. Mfumo wa jua B. mizazi C. Mazingira D. mkondo bahari
- iii. Mtindo wa Maisha unaohusisha asili, mila, desturi, jadi au itikadi inayotawala katika jamii huitwa?
A. Kimbunga B. Mazingira C. Uhusiano D. Utamaduni
- iv. Moja kati ya hizi zifuatazo siyo aina ya familia.
A. familia ya mzazi mmoja
B. familia ya wafugaji C. Familia mume na mke D. familia ya Watoto yatima
- v. Katika jamii, watu wanapoishi kwa kupendana, kuheshimiana na kusaidiana katika shughuli mbalimbali za kujiletea maendeleo huitwa?
A. utandawazi B. ukiritimba C. kujitegemea D. uhusiano mwema
- vi. Mimi naitwa mgandamizo wa hewa. Ninapimwa na kifaa kiitwacho?
A. Anemomita(Kilomita kwa saa B. Baromita (milibaa)
C. Kipimamvua (Milimita) D. Kipimawingu (Oktasi)
- vii. Moja kati ya shughuli za binadamu zifuatazo haisababishi uharibifu wa mazingira:
A. uchomaji mkaa B. ujenzi holela na utupaji taka ovyo
C. upandaji wa miti na nyasi D. moshi na kemikali kutokana na viwanda
- viii. Jumla ya vitu vyote vinavyotuzunguka, vyenye uhai na visivyo na uhai huitwa?
A. Mazingira B. vimondo na nyota C. Halijoto D. mizazi

2. Oanisha sentensi za fungu A na maneno ya fungu B kupata maana halisi.

N A	FUNGU A	JIBU	FUNGU B
i.	Vimiminika vinavyopatikana katika kipimajoto		A. Msitu B. Ramani
ii.	Ni chanzo cha asili cha joto		C. Obiti
iii.	Hujumuisha baba mama na Watoto wao		D. Jua
iv.	Mchoro wa kitu kama kinavyoonekana kutoka juu.		E. Familia ya awali.
v.	Sehemu ya ardhi iliyofunikwa na miti mingi na nyasi		F. Zebaki na alikoholi G. Mfumowa jua
vi.	Njia ya dunia kulizunguka jua.		

SEHEMU B: (Alama 22)

3. A. Jaza nafasi wazi kwa kuandika jibu sahihi

- i. Kaka wa mama yako mzazi unamwita nani? _____
- ii. Taja faida mbili za miti katika mazingira yako ya shule
(a) _____ (b) _____
- iii. Eneo kubwa na kame ambalo huwa na mchanga na lisiloota nyasi wala miti huitwa

- iv. Tanzania ni Muungano wa chi mbili ambazo ni _____ na

B. Kujibu kipengele cha (v) - (vii) andika **Ndiyo** kwenye maelezo yenye ukweli na **Hapana** kwenye maelezo yasiyo ya kweli.

- v. Hakuna umuhimu wa kutunza kumbukumbu za matukio yanayotokea katika familia

- vi. Mawingu hupimwa kwa kutumia kifaa kiitwacho kipimawingu na kipimio chake ni
oktasi _____
- vii. Julius Kambarage Nyerere alikuwa Waziri mkuu wa kwanza wa serikali ya Tanganyika
kuanzia Desemba 9, 1961 hadi Januari 22, 1962 _____
- viii. Jambo mojawapo la kudumisha utamaduni wa kitanzania ni kama vile kuvuta bangi

4. Jaza nafasi zilizoachwa wazi

- i. Jumla ya vitu vyote vinavyotuzunguka huitwa _____
- ii. Madini yanayochimbwa katika wilaya ya chunya huitwa _____
- iii. Zao la tumbaku ni zao la _____
- iv. Sayari tunayoishi huitwa ? _____

PRINTED BY NJALI N.M @2024

MAARIFA YA JAMII - MWONGOZO WA USAHIHISHAJI

SWALI	MAJIBU
1.	<ul style="list-style-type: none"> i. C ii. A iii. D iv. B v. D vi. B vii. C viii. A
2.	<ul style="list-style-type: none"> i. F ii. D iii. E iv. B v. A vi. C
3. A	<ul style="list-style-type: none"> i. Mjomba ii. Kivuli, hewa safi, kuni iii. Jangwa iv. Tanganyika na Zanzibar
B	<ul style="list-style-type: none"> v. Hapana vi. Kweli vii. Kweli viii. Hapana
4.	<ul style="list-style-type: none"> i. Mafuriko ii. Nyumba kuboka, vifo mifugo na binadamu iii. Mvua kubwa

